

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA

02 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA


KIKAO CHA THELATHINI NA SITA – TAREHE 02 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

316. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE
WAITARA (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Kata ya Kwihancha itapata Kituo cha Afya na ni lini huduma za afya zitaimarishwa katika Hospitali ya Nyamwaga.

317. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ukarabati wa Stendi Kuu ya Mabasi Bweri iliyopo Manispaa ya Musoma.

318. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa kuwa mfumo unawaacha nje Vijana wengi kwa kukosa sifa.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**319. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA
(KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuhamasisha kilimo cha zao la Mwani.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**320. MHESHIMIWA DKT. PAULINA DANIEL
NAHATO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza miundombinu ya Vyuo Vikuu nchini kutokana na ongezeko kubwa la Wanafunzi.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

321. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya Kambi ya Jeshi 845 Itaka na Wananchi wa Vijiji vya Sesenga na Itewe.



WIZARA YA AFYA:



322. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa bei elekezi ya vifaa vya tiba hasa vya macho, pua na koo.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

323. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Mto Ruvuma ili kufungua Shughuli za Kibiashara.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

324. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, ni lini Serikali itatunga Sheria ya Uanzishwaji wa Baraza la Taaluma kwa Kada ya Ustawi wa Jamii.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
02 JUNI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE